

HERI ALIYEMFANYA BWANA KUWA TUMAINI

Wimbo wa katikati
Jumapili ya 6, Mwaka C


Zab. 1: 1- 4, 6 (K) 39 : 5

Rogers K.J
February, 2025
Dodoma

He - ri a - li - ye-m fa - nya Bwa - na ku - wa tu - ma - i - ni la - ke,

wa - la ha - ku - wa - e - le - ke - a we - nye ki - bu - ri,

wa - la ha - ku - wa - e - le - ke - a we - nye ki - bu - ri.



1. Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki//
Wala hakusimama katika njia ya wakosaji;
Wala hakuketi barazani pa wenyewe mizaha,
Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo,
Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.
2. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji//
Uzaao matunda yake kwa majira yake;
Wala jani lake halinyauki,
Na kila alitendalo litafanikiwa.
3. Sivyo walivyo wasio haki//
Hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo,
Kwa kuwa Bwana anaijua njia ya wenyewe haki,
Bali njia ya wasio haki itapotea.